


Learning on TAP

# Upimaji wa uoni na usikivu kwa watoto wa umri wa shule

## Maneno muhimu: Usikivu na afya ya kusika kwa watoto

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Odiomita** | Kifaa kinachotumika kupima usikivu. |  |
| **Kipimo cha usikivu** | Kipimo ambacho mpimwaji anavaa hedifoni na kusikiliza sauti mbalimbali ili kujua kama anasikia vizuri. Kama kuna upotevu wa sauti, matokeo yataonyesha ukubwa wa  tatizo. |  |
| **Utando wa ngoma ya sikio** | Ni ni kiungo chembamba ambacho kinatenganisha sikio la nje na la ndani na kiungo hiki kinalinda sehemu ya ndani ya sikio dhidi ya maambukizi. |  |
| **Kitu kutoka nje ya mwili** | Kitu kischohitajika ndani ya mwili ambacho kimekwama sehemu ya mwili lakini hakikupaswa kuwepo eneo kilichopo. Kwa mfano, chembe ya udongo iliyo chini ya kope la jicho au mdudu aliye katika njia ya sikio |  |
| **Masafa** | Masafa ni idadi ya kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti ndani ya sekunde moja. Kuna aina tofauti za sauti ikiwemo sauti nzito ( masafa ya chini) mfano, sauti nzito na sauti kali ( masafa ya juu) kwa mfano filimbi. Masafa yanapimwa kwa kutumia kipimo cha Hezi (Hz) |  |
| **Kifaa saidizi cha usikivu** | Kifaa kinachovaliwa kwenye sikio na watu wenye upotevu wa usikivu. Kifaa saidizi cha usikivu kinafanya sauti isikike kwa nguvu ili mtu huyo mwenye upotevu wa usikivu, aweze kusikia, kuwasiliana na kushiriki zaidi kwenye shughuli zake za kila siku. |  |
| **Otoskopi** | Kifaa cha kuongeza ukubwa wa kitu. Kifaa hiki kina mwanga kwa mbele ili kuweza kukagua sikio la mgonjwa. |  |
| **Mfanyakazi** | Watu wanaofanya kazi kwenye sehemu ya kutoa huduma au taasisi. Watu hawa ni pamoja na wale waliopata mafunzo maalumu ya  kutoa huduma za afya ambao yawezekana wasiwe na vigezo vya kitaaluma | |

| | | |
|---|---|---|
| **Kifaa maalum cha kutanua viungo (Spekulamu)** | Sehemu ya mbele ya Otoskopi, inayowekwa ndani ya sikio la mtoto. |  |